

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 41 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** JULAI 2024

MWENYEKITI NA WAJUMBE WA TSC WAAPISHWA NA KUANZA KAZI RASMI



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Prof. Maosud Hadi Muruke kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma tarehe 13 Juni, 2024.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

KONGOLE WAJUMBE WA TSC KWA KUANZA KAZI KWA KISHINDO

Tarehe 13 Juni, 2024 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alimuapisha Prof. Masoud Hadi Muruke ili kuanza kutekeleza majukumu ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Mara baada ya uapisho wa Prof. Muruke, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed O. Mchengerwa (Mb) aliwaapisha Makamishna nane (8) aliowateua kuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Siku hiyohiyo, Makamishna/Wajumbe hao wa Tume waliingia katika utekelezaji wa majukumu ya TSC kwa kuanza Mkutano wa Tume ambao ulifanyika kwa siku mbili. Katika mkutano huo Kamati zote za Wilaya ziliteuliwa, maombi ya walimu 32 ambao waliomba kuajiriwa upya katika Utumishi wa Umma

yalifanyiwa kazi, Kamati za Tume ziliundwa na wajumbe wake kuteuliwa, na Mwenyekiti wa Tume kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za TSC na kutoa maagizo kwa mkandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Juhudi hizo zinaonesha namna ambavyo Makamishna hao walivyodhamiria kuisaidia Tume kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ubora. Matokeo ya kazi yao tayari yameanza kuonekana katika Ofisi za Tume ngazi ya Wilaya ambapo Kamati zilizoteuliwa tayari zimeanza kufanya kazi za kuamua masuala mbalimbali ya walimu ikiwemo upandishaji vyeo.

Tuna imani kubwa kuwa Makamishna wa Tume wataiwezesha TSC kufikia malengo yake kwa haraka katika kusimamia Ajira, Nidhamu na Maendeleo ya Walimu kote nchini.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent

Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



tumeyautumishiwawalimutanzania

MWENYEKITI NA WAJUMBE WA TSC WAAPISHWA NA KUANZA KAZI RASMI

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 13 Juni, 2024 aliwaapisha viongozi mbalimbali aliowateuwa hivi karibuni katika hafla iliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma.

Miongoni mwa viongozi walioapishwa ni Prof. Masoud Hadi Muruke ambaye Rais Samia alimteua tarehe 15 Mei, 2024 kuwa mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) akichukua nafasi ya Prof. Willy Lazaro Komba ambaye muda wake ulimalizika.

Mara baada ya Rais Samia kumuapisha Mwenyekiti wa Tume, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed O. Mchengerwa (Mb) aliwaapisha Makamishna nane (8) aliowateua

hivi karibuni kuwa wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Waziri alifanya uapisho huo tarehe 13, Juni 2024 katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma ambapo walioapishwa ni Bi. Mariam Gerald Mwanilwa kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Huruma Elias Mageni kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, Bi. Hadija Mcheka kutoka OR – TAMISEMI na Bi. Mariam Rashid Haji kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Wajumbe wengine ni Bi. Bahati Shabani Mgongolwa kutoka Wizara ya Fedha, Bw. Agrey Adelbert Mleli kutoka Baraza la Taifa la Ufundi na Mafunzo (NACTVET), Bi. Jane Nikusomoka Mtindya kutoka Chama cha Walimu Tanzania na Bw. Lameck

Philipo Mahewa kutoka Chama cha Walimu Tanzania.

Akizungumza katika hafla hiyo, Waziri Mchengerwa alimtaja Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wa Tume hiyo kuhakikisha wanamaliza kero na changamoto za walimu ikiwemo ucheleweshwaji wa kupandishwa madaraja na walimu kucheleweshwa kubadilishiwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu.

Waziri Mchengerwa alisema anaimani kuwa viongozi hao watafanya maboresho makubwa katika utumishi wa walimu ili walimu waendeleo kufanya kazi kwa amani na utulivu huku akisisitiza kuwa nia ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuona changamoto zote za walimu zinamalizwa na walimu wanatendewa haki kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

“Tunakupongeza Prof. Muruke kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, sisi tunakuamini. Walimu ni watu muhimu sana kwenye Taifa letu, na wewe umeletwa hapa makusudi ili kwa kushirikiana na Wajumbe na Sekretarieti ya Tume mfanye maboresho makubwa ili kumaliza changamoto za walimu. Sitarajii kusikia kwenye kijiji, kitongoji au shule yoyote kuna mwalimu ambaye changamoto zake hazijashughulikiwa,” alisema Waziri Mchengerwa.

Mara baada ya uapisho, Wajumbe hao wa Tume wameingia katika utekelezaji wa majukumu ya TSC kwa kuanza Mkutano wa Tume unaofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete ambapo masuala mbalimbali ya yanayohusu utumishi wa walimu yalihamuliwa.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bi. Mariam Gerald Mwanilwa kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.

MWENYEKITI NA WAJUMBE WA TSC WAAPISHWA NA KUANZA KAZI RASMI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bw. Huruma Elias Mageni kutoka Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bi. Hadija Mcheke kutoka OR – TAMISEMI kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bi. Mariam Rashid Haji kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bi. Bahati Shabani Mgongolwa kutoka Wizara ya Fedha kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.

MWENYEKITI NA WAJUMBE WA TSC WAAPISHWA NA KUANZA KAZI RASMI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bw. Aggrey Adelbert Mleli kutoka Baraza la Taifa la Ufundi na Mafunzo (NACTVET) kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bi. Jane Nikusomoka Mtindya kutoka Chama cha Walimu Tanzania kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) akimuapisha Bw. Lameck Philipo Mahewa kutoka Chama cha Walimu Tanzania kuwa Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi za OR – TAMISEMI zilizopo jengo la Sokoine jijini Dodoma.

MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAFANYIKA KWA SIKU MBILI, WAJUMBE WA KAMATI ZA WILAYA WATEULIWA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ulifanyika kwa siku mbili tarehe 13 na 14 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma ambapo pamoja na mambo mengine Kamati zote za Wilaya zimeteuliwa.

Mkutano huo ulioongozwa na Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke ulianza tarehe 13 Juni 2024, ikiwa ni saa chache baada ya Prof. Muruke kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kushika nafasi hiyo na Makamishna (wajumbe) wa Tume kuapishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mhe. Mohamed O. Mchengerwa (Mb). Katibu wa Mkutano huo ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

Katika Mkutano huo, Wajumbe wa Tume walifanikiwa kuteua Wajumbe wa Kamati za Wilaya ambao kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448 kamati hizo ndizo zenye mamlaka ya kufanya maamuzi ya masuala ya kiutumishi ya walimu ikiwemo kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo, kubadilisha cheo/kazi waliojiendeleza kielimu pamoja na kushughulikia masuala ya nidhamu kwa walimu.

Hivyo, kuteuliwa kwa Kamati za Wilaya kunaziwezesha Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya kutekeleza majukumu yake yote kikamilifu.

Pamoja na hilo, Mkutano wa Tume ulipokea na kufanyia kazi maombi ya walimu 32 ambao wameomba kuajiriwa upya katika Utumishi wa Umma baada ya kutumikia adhabu ya kufukuzwa kazi kwa miezi isiyopungua 12 (mwaka mmoja).

Wakati huo huo Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke aliteua Wajumbe wa Kamati tatu



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Maosud Hadi Muruke akiongoza Mkutano wa Tume uliofanyika kwa siku mbili (2), tarehe 13 hadi 14 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma

(3) za Tume ambao ni miongoni mwa Makamishna wa Tume hiyo. Kamati hizo ni Kamati ya Maadili na Nidhamu, Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu na Kamati ya Fedha, Utawala, Utafiti na Elimu kwa Umma.

Kamati ya Maadili na Nidhamu itaongozwa na Jane Mtindya huku wajumbe wake wakiwa ni Mariam Haji na Huruma Mageni. Kamati

ya Ajira na Maendeleo ya Walimu itaongozwa na Khadija Mcheka na Wajumbe wake ni Lameck Mahewa na Mariam Mwanilwa. Kamati ya Fedha, Utawala, Utafiti na Elimu kwa Umma itaongozwa na Mariam Mwanilwa na wajumbe wake ni Bahati Mgongolwa na Aggrey Mleli. Katibu wa Kamati zote tatu ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

MKUTANO WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAFANYIKA KWA SIKU MBILI, WAJUMBE WA KAMATI ZA WILAYA WATEULIWA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa wasilisho juu ya taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya TSC kwenye Mkutano wa Tume uliofanyika kwa siku mbili (2), tarehe 13 hadi 14 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.



Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) chini ya Mwenyekiti, Prof. Maosud Hadi Muruke ukiwa unaendelea tarehe 14 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Baadhi ya Washiriki wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika Mkutano huo tarehe 14 Juni, 2024 katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

KATIBU MKUU IKULU AWATAKA WASIMAMIZI WA SHERIA KUTATUA MALALAMIKO YA WATUMISHI DHIDI YA SERIKALI



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Bw. Mululi Mahendeka akifungua mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.

Na Mwandishi wetu – Morogoro.

Katibu Mkuu Ofisi Ikulu Bw. Mululi Mahendeka amewataka Wasimamizi wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma kufanya kazi ya kuondoa kero na malalamiko kutoka kwa watumishi na wananchi dhidi ya Serikali.

Ametoa kauli hiyo hivi karibuni mjini Morogoro wakati akifungua mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma.

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwambusha na kuwaelimisha kuhusu uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, hususan kwenye usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya nidhamu, malalamiko, rufaa na kero za watumishi wa Umma na wananchi

“Ili Taifa letu liweze kuendelea, hatuna budi kufanya kazi ya ziada kuondoa kero na malalamiko dhidi ya Serikali kutoka kwa watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla...kwa kutambua umuhimu wa suala hili, Serikali imeendelea kufanya maboresho

katika Sekta ya Umma ili kuona kwamba sekta hii inatoa huduma bora na kwa haraka kwa wateja wake wote,” alisema.

Aliwataka kubadilika na kuwa wasimamizi mahiri wa rasilimaliwatu, kuwa waadilifu na wenye mwenendo mzuri mahali pa kazi na nje ya maeneo ya kazi ili kuleta ufanisi katika matumizi ya rasilimali nyingine na kuwezesha Ofisi za umma kutoa huduma bora zaidi.

“Naelewa kuwa malalamiko hayawezi kukosekana katika jamii yoyote na kwamba siyo sahihi kuzuia malalamiko ila tunao wajibu wa kuwa na utaratibu na mbinu nzuri ya kushughulikia malalamiko na kuyapatia ufumbuzi,” alisema.

Alisema kuwa, wanaposhindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo kwenye ofisi zao, inasababisha kazi hizo zipelekwe kwa viongozi wa juu akiwamo Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Katibu Mkuu Kiongozi ili wazifanye kwa niaba yao.

“Kumbukeni daima kwamba, huo ni ukiukaji wa sheria na ni utovu wa nidhamu ambao hauvumiliki... Sasa, naagiza msielelee kufanya hivyo tena... masuala yaliyo katika uwezo wenu myamalize ninyi wenyewe kwa haraka na kwa usahihi,”

aliwaagiza.

Bw. Mahendeka alisema kuwa pale wanapoona hawana uhakika na kile wanachopaswa kufanya juu ya suala lililo mbele yao, walisikukumie ngazi nyingine au kumuaacha mwananchi husika bila msaada, bali watafute ushauri kwa watumishi wenzao.

Alisema kuwa mtumishi yeyote atakayebainika kuwa ni chimbuko la matatizo kwenye taasisi yake ataundiwa Kamati ya Uchunguzi na hatua stahiki zitachukuliwa kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

Bw. Mahendeka alisisitiza kuwa hatua stahiki zitakozochukuliwa zitahusisha taasisi za umma zinazozalisha malalamiko mengi yasiyopatiwa ufumbuzi kwa muda mrefu, taasisi zisizowasilisha taarifa au zinazochelewa kuwasilisha taarifa wanazoombwa.

Aliongeza kuwa Watumishi wa Umma wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanawatumikia wananchi kwa kutoa huduma nzuri, huku wakifahamu kuwa wateja wao ni wananchi ambao wanatarajia huduma bora kutoka kwao.

“Wananchi nje ya sekta ya Umma wanafahamu kabisa kuwa watumishi wa Umma walio katika taasisi na ofisi mbalimbali za Umma ni watoa huduma, ambazo wananchi wanazihitaji na wana haki ya kuzipata,” alisema.

Bw. Mahendeka alisema wanapowahudumia wananchi wanapaswa kujua majukumu yao ipasavyo, kujua haki na wajibu, mazingira ambayo wananchi hao wanaishi na mahitaji yao muhimu, ili kurahisisha kupata ufumbuzi wa matatizo, malalamiko, kero na changamoto zao.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu Ikulu, Bw. Mahendeka alisema usimamizi wa masuala ya nidhamu katika Utumishi wa Umma unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298.

Alisema Sheria hiyo inatoa

KATIBU MKUU IKULU AWATAKA WASIMAMIZI WA SHERIA KUTATUA MALALAMIKO YA WATUMISHI DHIDI YA SERIKALI

uwezo kwa mamlaka mbalimbali za nidhamu na rufaa katika Utumishi wa Umma na kuweka misingi ya namna masuala hayo yanavyopaswa kushughulikiwa.

Bw. Mahendeka aliongeza kuwa ili kutekeleza vyema majukumu yao wanapaswa kujua vyema sheria hiyo, kanuni zake na miongozo iliyotungwa chini ya sheria hiyo inayohusu masuala ya nidhamu na rufaa kwa watumishi wa Umma.

Alisema kuwa kupitia hoja za rufaa zinazowasilishwa na Warufani kwa Rais, imebainika Warufani wanaulewa mzuri wa haki zao za msingi kisheria na wanajikita kwenye kanuni zilizokiukwa.

Aidha, Bw. Mahendeka alisema usimamizi wa Maadili na Nidhamu ya Watumishi wa Umma unategemea uwepo wa uelewa wa pamoja kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo iliyowekwa ili kutekelezwa na viongozi waliopewa dhamana ya kuwasimamia watumishi.

Alisema kuwa mojawapo ya changamoto inayosababisha watumishi wa Umma kukiuka



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bw. Adolf Ndunguru akitoa maelezo mafupi kabla ya hajamkaribisha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Bw. Mululi Mahendeka (hayupo katika picha) afungue mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.

maadili ya kazi, ni pamoja na Mamlaka zao za Nidhamu

kutokujua majukumu yao ipasavyo na hivyo kuwa na uelewa tofauti wanaposhughulikia masuala ya kinidhamu ya watumishi.

Bw. Mahendeka alisema kuwa hali hiyo pia inasababisha kuwepo kwa malalamiko na rufaa nyingi za mashauri ya nidhamu katika ngazi za juu za uongozi zinazotokana na maamuzi yasiyozingatia sheria, kanuni, taratibu na maelekezo mbalimbali.

Alisisitiza kuwa usimamizi mzuri wa maadili na nidhamu kwa watumishi wa Umma na kufanyia kazi malalamiko ya wananchi kwa ufanisi, unawezesha Serikali kufikia malengo yake ikiwa ni pamoja na kufanikisha Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Bw. Mahendeka alisema kuwa usimamizi mzuri wa maadili ya watumishi wa Umma utasaidia kuwa na watumishi waadilifu, wawajibikaji, wanaofanya kazi kwa uwazi na wanaotumia vizuri Rasilimali zilizopo na kuwa na wananchi wanaoiamini Serikali na kushiriki vyema katika shughuli za maendeleo kwa kufuata miongozo mbalimbali inayotolewa.

Aliwataka kuzingatia sheria katika kutekeleza majukumu yao, uadilifu, uaminifu, kujituma, kuwaheshimu na kuwathamini wateja wote mnaopaswa kuwahudumia na kuongeza kuwa utendaji wowote usiozingatia hayo, husababisha malalamiko na rufaa mara kwa mara.

Bw. Mahendeka alisema kuwa malalamiko na rufaa nyingi ambazo zimekuwa zikifikishwa Ikulu, kutoka kwa wananchi na watumishi wa Umma, zinatokana na utendaji usiozingatia umakini, kutokujali na kuelewa mazingira na mahitaji ya huduma ya mteja, kutozingatia sheria, kukosa uadilifu, kukosa uaminifu, kutojituma, kutoheshimu na kutothamini wale wanaohitaji kuhudumiwa.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo mafupi wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.

KATIBU IKULU AWATAKA WASIMAMIZI WA SHERIA KUTATUA MALALAMIKO YA WATUMISHI DHIDI YA SERIKALI



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akibadilishana mazwazo na baadhi ya watumishi wa TSC waliokuwa wakihudhuria mafunzo ya wiki moja kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma wakifuatilia hotuba ya ufunguzi hivi karibuni mkoani Morogoro.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu Bw. Mululi Mahendeka (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi na washiriki wa mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Bw. Mululi Mahendeka (kushoto) akibadilishana mawazo na viongozi mbalimbali mara baada ya kufungua mafunzo kwa baadhi ya Watumishi wa Umma wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma hivi karibuni mkoani Morogoro.

MWL. PAULINA: VIONGOZI MNAOSIMAMIA WALIMU SHUGHULIKIENI KERO ZAO



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, CPA Hawa Hassan (katikati) akizungumza na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (kulia) na ujumbe kabla hajazungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kiteto hivi karibuni.

Na Mwandishi Wetu – Kiteto.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama aliwataka Maafisa wa Halmashauri wanaohusika kushughulikia maslahi ya Walimu kuhakikisha wanabaini changamoto kwa ajili ya kutafutiwa ufumbuzi ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao katika mazingira rafiki.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa mkutano wake na Walimu kutoka Halmashauri za Wilaya ya Kiteto ambapo alieleza kuwa Maafisa Elimu wa Wilaya wa Shule za Msingi na Sekondari, Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kushirikiana na Maafisa Utumishi wanapaswa kuingia katika Mfumo na kuona kama kuna walimu wenye changamoto mbalimbali za madai na kuhakikisha viambatana vyao vinavyohitajika vimo ili walimu waweze kulipwa haki zao kwa wale wanaostahili.

Alisema kuwa Viongozi hawategemei kusikia Maafisa Elimu wa Wilaya wakiwaagiza Walimu

wanapokuwa na changamoto kufuatilia haki zao au madai kwa Maafisa Utumishi badala yake wanatakiwa kuendelea na jukumu la kuwalea na kuwapa ujuzi wanafunzi.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa Maafisa hao wanapokuwa wamekamilisha na kupata uhakika ni vyema wakawasiliana na walimu husika juu ya madai yao kama yanastahili kulipwa na kama wameshalipwa ni vizuri wakiwaeleza ili wajue hatua

iliyofikiwa katika kushughukia changamoto zao.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Haasan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitaki kusikia walimu wanakabiliwa na changamoto ambazo zinawavunja nguvu katika utoaji elimu kwa wanafunzi.

Aidha, Mwl. Paulina aliwashauri Walimu kutokubali kutoa kadi zao za Benki (ATM CARD) kwa watu wanaowakopesha ili kuepuka kudhalilishwa na wakati mwingine kudhulumiwa na watu ambao wanawakopesha bila kuwa na vibali halali.

Alisema kuwa hivi sasa Serikali ya Awamu ya Sita imeweka mazingira mazuri ya kukopesha kupitia mikopo ya Hazina na Taasisi za Benki ambazo inazitambua kupitia mikopo kwa njia ya mtandao (e-Loan) ambapo watumishi wakiwemo walimu wananufaika na mikopo hiyo.

Ziara hiyo ya kukutana na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari inaendelea katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutoa mikakati ya kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu nchini.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kuimba wimbo wa Taifa hivi karibuni katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kiteto kabla ya kuanza mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya hiyo.

MWL. PAULINA: VIONGOZI MNAOSIMAMIA WALIMU SHUGHULIKIENI KERO ZAO



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kiteto wakiimba wimbo wa Taifa kabla ya mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) hivi karibuni katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kiteto.



Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Manyara Bw. Mugisha Galibona akitoa salamu za Mkoa hivi karibuni wilayani Kiteto kabla ya mkutano wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Kiteto wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) hivi karibuni katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Kiteto.



Mkuu wa Shule ya Sekondari Matui wilayani Kiteto, Dkt. Japhet Kivuyo akitoa neno la shukurani baada ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (katikati meza kuu) kuzungumza na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kiteto hivi karibuni.

SERIKALI YA AWAMU YA SITA INAAMINI KATIKA KUWEKEZA KWENYE MICHEZO: WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA

Na Mwandishi wetu – Tabora.

Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa, tarehe 8 Juni 2024 alifungua rasmi Michezo ya Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) pamoja na ile ya shule za Sekondari (UMISSETA) ambayo inafanyika Kitaifa Mkoani Tabora.

Waziri Mkuu alifungua mashindano hayo katika Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi Mjini Tabora, huku akisisitiza kuwa Serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaamini kwenye uwekezaji katika michezo ya wanafunzi wa shule ya Msingi na Sekondari Nchini.

“Mhe. Rais Dkt. Samia suluhu Hassana anawapenda sana na anayo matumaini makubwa kuwa, michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA itaendelea kuwa dirisha la matumaini katika kuimarisha na kuinua viwango vya michezo hapa nchini kwa kutoa wanamichezo bora hivyo anawatakiwa kila la kheri katika michezo hii”

“Serikali inaamini katika uwekezaji kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, uwekezaji huu unachagia kwa asilimia kubwa maandalizi ya wachezaji wenye umahiri ambao pia wataweza kufanya vizuri ndani na nje ya nchi na hii ndio maana hasa ya uwepo wa michezo hii katika ngazi ya Taifa” amesema Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu pia aliwataka wazazi na jamii kwa ujumla kuhakikisha inawasaidia watoto kushiriki na kukuza vipaji vyao kwenye michezo ili wafaidike na fursa zilizopo kwenye michezo katika dunia ya sasa.

“Kwa upande wa wazazi na

walezi, hakikisheni na himizeni ushiriki wa watoto katika michezo na sanaa ili wasijitenge na fursa zinazopatikana katika dunia ya sasa.”

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa alieleza umuhimu wa mashindano hayo katika kukuza michezo na vipaji nchini, ikiwa ni sehemu ya uwekezaji michezoni ambao utalisaidia taifa katika siku zijazo.

Mhe. Mchengerwa alisema kuwa baada ya kumalizika kwa mashindano ya mwaka huu kutafanyika uzinduzi wa timu za Taifa zitakazotokana na michezo ya UMITASHUMTA & UMISSETA 2024, ambao unalenga kuandaa wachezaji watakaotumikia Taifa katika siku za mbeleni.

“Hivi karibuni baada ya Mashindano haya, tutazindua timu za taifa za vijana hawa, ni

jukumu la vijana kuhakikisha wanatumia welediwa wote katika mashindano haya tuone ujuzi wao wote kuhakikisha kwamba miongoni mwao wapatikane wachezaji watakaounda timu hizi za Taifa ambazo tutazitaja baada ya mashindano haya” amesema Mchengerwa.

Naye Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Damas Ndumbaro amesema Tanzania imeandaa mashindano mapya yaliyopewa jina la ‘Mwalimu Nyerere Liberation Cup’ ambayo yatakuwa ni mashindano ya vijana wenye umri wa miaka chini ya 20 yatakayojumuisha Bara lote la Afrika.

“Tutaweka michezo ya aina mbalimbali na sisi Tanzania ndio wenyeji kwa hiyo vijana watakaotoka kwenye mashindano haya (UMITASHUMTA na UMISSETA) watahusika katika kombe hilo,” amesema Dkt. Ndumbaro.

Ufunguzi wa Mashindano hayo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwemo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.



Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akitoa hutuba ya ufunguzi wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) pamoja na ile ya shule za Sekondari (UMISSETA) tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora.

SERIKALI YA AWAMU YA SITA INAAMINI KATIKA KUWEKEZA KWENYE MICHEZO: WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) (kulia) akitoa burudani ya muziki pamoja na wanafunzi wanamichezo wenye ulemavu wa kusikia wakati wa uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA uliofanyika tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye mirwani) akiwa pamoja na viongozi mbalimbali wakati wa uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA uliofanyika tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora.

**SERIKALI YA AWAMU YA SITA INAAMINI KATIKA KUWEKEZA
KWENYE MICHEZO: WAZIRI MKUU KASSIM MAJALIWA**

Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akipuliza kipyenga kuashiria ufunguzi rasmi wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) pamoja na ile ya shule za Sekondari (UMISSETA) tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora.



Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akiwasili katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora kwa ajili ya ufunguzi rasmi wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) pamoja na ile ya shule za Sekondari (UMISSETA) tarehe 8 Juni, 2024.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb) (kulia) akimsikiliza Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) wakati wa uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA uliofanyika tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora.



Wanafunzi wanaoshiriki michezo wakiwa katika uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora wakati wa uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA tarehe 8 Juni, 2024.



Wanafunzi waliohudhuria uzinduzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA tarehe 8 Juni, 2024 mkoani Tabora wakiimba wimbo wa mashindano hayo.

MWL. PAULINA: SERIKALI IMEWEKA MFUMO MZURI WA KUWAEPUSHA NA MIKOPO UMIZA

**Na Mwandishi Wetu –
Simanjiro.**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama aliwataka walimu kutumia dirisha lililoanzishwa kwenye Mfumo wa Upimaji wa Utendaji kazi kwa Watumishi (ESS) wanapohitaji kuomba mikopo isiyomiza.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa mkutano wake na Walimu kutoka Halmashauri za Wilaya ya Simanjiro wakati akizungumza na Walimu wa Shule ya Msingi na Sekondari kuhusu mbinu na mikakati ya uboreshaji wa elimu.

Mwl. Paulina alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka utaratibu mzuri kwa watumishi kukopa kwa kuanzisha Dirisha hilo la Mkopo kwa njia ya Mtandao (e-loan) kwa ajili ya kuwaondolea watumishi



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kuimba wimbo wa Taifa hivi karibuni kabla ya kuanza mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari

changamoto ya kukimbilia Taasisi zisizo rasmi za ukopeshaji.

Alisema kuwa kupitia dirisha hilo Serikali imeingia mkataba na Benki kama CRDB, NMB, NBC na benki nyingine nchini kuwawezesha Watumishi wa umma wakiwemo walimu

mtandao kuomba mikopo.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa kutokana na juhudi hizo za Serikali walimu wanapaswa kuachana na mikopo umiza ambayo inasababisha wadhalilike na kupoteza heshima yao ambapo baadhi yao wamekuwa wakikabidhi kadi zao za benki jambo ambalo linawafanya baadhi kuishi maisha duni.

“Serikali ya Awamu ya Sita imeleta mwarobaini wa kuachana na mikopo umiza au kausha damu ambayo ilikuwa ikitesa walimu na watumishi wengine... tuchangamkie fursa hiyo walimu wenzangu...nywila na kadi ni mali ya mhusika (Mwalimu) na hivyo ni marufuku kwa Mwalimu kutoa kadi yake na nywila kwa mtu,” alisema.

Ziara hiyo ya kukutana na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari inaendelea katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kutoa mikakati ya kuleta mabadiliko makubwa kwenye sekta ya elimu nchini.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro hivi karibuni.

MWL. PAULINA: SERIKALI IMEWEKA MFUMO MZURI WA KUWAEPUSHA NA MIKOPO UMIZA



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani Simanjiro wakiimba wimbo wa Taifa kabla ya mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) hivi karibuni.



Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Manyara, Bw. Mugisha Galibona akitoa salamu za Mkoa hivi karibuni wilayani Simanjiro kabla ya mkutano wa walimu wa Shule za Msingi na Sekondari.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro hivi karibuni.

Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari Wilayani Simanjiro wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) hivi karibuni.

PROF. MURUKE AKERWA NA KASI NDOGO UJENZI WA JENGO LA TSC MAKAO MAKUU, AAGIZA KAZI IFANYIKE USIKU NA MCHANA

Na Mwandishi wetu – TSC.

Mwenyeekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke tarehe 15 Juni, 2024 alitembelea na kukagua maendeleo ya mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za TSC Makao Makuu linalojengwa katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma na kuonesha kutoridhishwa na kasi ya ujenzi huo.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Muruke alimtaka mkandarasi SUMA JKT kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha kuwa mradi huo unakamilika kabla au ifikapo mwezi Desemba 2024 ikiwa ni muda wa nyongeza baada ya muda wa awali kumalizika huku ujenzi huo ukiwa umefikia asilimia 48 tu.

“Ujenzi wa mradi huu hauendi kwa kasi inayotakiwa kulingana

na makubaliano yaliyomo katika mkataba, miezi 18 tuliyokubaliana awali kuwa ujenzi utakamilika imemalizika na kazi ndio ipo asilimia 48. Mmeomba nyongeza ya muda wa miezi sita ili kukamilisha ujenzi, lakini kasi mnayokwenda nayo bado hairidhishi,” alisema Prof. Muruke.

Alisisitiza kwa kusema, “Fanyeni kazi usiku na mchana na muongeze idadi ya mafundi ili kazi ikamilike katika muda mliomba... tunazihitaji sana hizi Ofisi ili tuweze kutoa huduma katika mazingira mazuri kwa walimu ambao ndio kundi kubwa la watumishi wa umma...mimi nitajitahidi kuja mara kwa mara kuona maendeleo ya mradi huu.”

Awali akitoa taarifa ya maendeleo ya mradi huo, Mhandisi kutoka SUMA JKT Bw. Aminiel Kishebuka, alisema kuwa ujenzi wa mradi huo ulikuwa

ukamilike mwezi Juni mwaka huu lakini kutoka changamoto mbalimbali wamelazimika kuomba kuongezewa muda hadi Desemba 2024.

Alisema kuwa ujenzi wa mradi huo umefikia asilimia 48 na kuongeza kuwa watafanya kila linalowezekana ili mradi huo ukamilike ndani ya muda wa nyongeza.

Mwenyeekiti huyo aliongozana na baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Tume hiyo akiwemo Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama, Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Fatuma Muya, Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA, Bi. Kainda Ndasa, Mkurugenzi Msaidizi wa Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Mectildis Kapinga na Mkurugenzi Msaidizi wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Bi. Eliainenyi Mariki.



Mwenyeekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akiangalia mchoro wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu alipotembelea ujezi wa ofisi hizo tarehe 15 Juni, 2024 katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma. Kushoto ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

PROF. MURUKE AKERWA NA KASI NDOGO UJENZI WA JENGO LA TSC MAKAO MAKUU, AAGIZA KAZI IFANYIKE USIKU NA MCHANA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Hadi Muruke (wa nne kutoka kulia) wakati mwenyekiti huyo alipotembelea ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu unaoendelea eneo la Njedengwa jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akielekea kukagua Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Katikati ni Mhandisi kutoka SUMA JKT, Bw. Aminiel Kishebuka na kulia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akimuonyesha jambo Msimamizi wa Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mhandisi kutoka SUMA JKT, Bw. Aminiel Kishebuka (kulia) wakati alipotembelea ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu unaoendelea mjini Dodoma. Nyuma yao ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (kushoto) akimuonyesha jambo Msimamizi wa Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mhandisi kutoka SUMA JKT, Bw. Aminiel Kishebuka (kulia) wakati alipotembelea ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Makao Makuu unaoendelea mjini Dodoma. Nyuma yao ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama.

PROF. MURUKE AKERWA NA KASI NDOGO UJENZI WA JENGO LA TSC MAKAO MAKUU, AAGIZA KAZI IFANYIKE USIKU NA MCHANA



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (mbele) akielekea kukagua Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC). Katikati ni Mhandisi kutoka SUMA JKT, Aminiel Kishebuka na kulia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (aliyeshika nguzo) akitoa maelekezo kwa msimazi wa Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mhandisi kutoka SUMA JKT, Aminiel Kishebuka (aliyegeuka).



Msimamizi wa Mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mhandisi kutoka SUMA JKT, Aminiel Kishebuka (kushoto) akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) wakati alipotembelea mradi huo tarehe 15 Juni, 2024. Kulia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

Msimamizi wa Mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mhandisi kutoka SUMA JKT, Aminiel Kishebuka (aliyenyoosha mkono) akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Masoud Hadi Muruke (katikati) wakati alipotembelea mradi huo tarehe 15 Juni, 2024. Kulia ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.

PROF. MURUKE AKERWA NA KASI NDOGO UJENZI WA JENGO LA TSC MAKAO MAKUU, AAGIZA KAZI IFANYIKE USIKU NA MCHANA

Msimamizi wa Mradi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mhandisi kutoka SUMA JKT, Aminiel Kishebuka (aliyenyoosha mkono) akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (wa tatu kutoka kushoto) wakati alipotembelea mradi huo tarehe 15 Juni, 2024. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (aliyeshika nondo) akikahikisha usalama wa nguzo wakati alipotembelea Mradi wa ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mjini Dodoma tarehe 15 Juni, 2024.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Hadi Muruke (kulia) akibadilishana marwazo na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) mara baada ya kukagua mradi wa ujenzi wa Ofisi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) mjini Dodoma tarehe 15 Juni, 2024.

WAZIRI SIMBACHAWENE AFUNGUA MAONESHU YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb) tarehe 19 Juni, 2024 alifungua maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.

Akifungua maadhidhisho hayo, Waziri Simbachawene aliwaagiza Watumishi wa Umma ambao bado hawajajisajili kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji wa Kazi wa Watumishi wa Umma (PEPMIS) kuhakikisha wanajisajili kwenye mfumo huo ndani ya wiki moja ili kutii maagizo ya Serikali.

Waziri huyo alisema Ofisi yake imeshaweka utaratibu kwa kila mtumishi kuweza kujisajili na kupata huduma kupitia mfumo huo hivyo hakuna kisingizio kwa mtumishi yeyote kutofanya hivyo.

“Agizo langu la kwanza ni kwamba Watumishi wa Umma ambao bado hawajajisajili kwenye mfumo wa PEPMIS wahakikishe wanajisajili ndani ya wiki hii. Kwa wale ambao wapo masomoni, Ofisi yangu imeshatoa utaratibu wa nini

kifanyike, hivyo hakuna sababu ya Mtumishi wa Umma kutojijisajili kwenye mfumo huo,” alielekeza Waziri Simbachawene.

Vilevile kiongozi huyo, aliagiza Watumishi wa Umma kutumia mifumo ya TEHAMA ya Serikali katika utekelezaji wa majukumu yao ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na kupunguza gharama za matumizi ya karatasi ofisini.

Sambamba na hilo, Waziri hiyo ameagiza Wizara na Taasisi zote za Serikali kutumia mifumo ya TEHAMA ya Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi ili kuongeza ufanisi katika kutoa huduma na kuepusha upotevu wa muda, usumbufu na urasimu kwa mwanachi.

“Lengo la Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora inayokidhi matarajio yao, na kwa kuliona hilo Serikali imeweka nguvu zaidi kwenye matumizi ya teknolojia ili kuendana na mabadiliko yanayotokea duniani. Hivyo, ninazielekeza Taasisi zote za Serikali kutumia mifumo ya TEHAMA tuliyonayo katika kuwahudumia wananchi,” alisema Waziri Simbachawene.

Agizo lingine alilotoa Waziri huyo ni Taasisi za Umma kufanya

shughuli za kijamii hususan katika maeneo ambayo wananchi wanapata huduma kama vile hospitali, magerezani, nk. kwani kwa kufanya hivyo kunasaidia kuimarisha ushusiano kati ya Serikali na wananchi wake.

Kiongozi huyo, alihitimisha kwa kuziagiza Taasisi zote kufanya tathmini kupitia mrejesho wanaoupata kutoka kwa wateja wanatembelea mabanda yao na tathmini hiyo isaidie taasisi husika kufanya maboresho katika kutoa huduma kwa wananchi.

“Sambamba na hilo ninazielekeza kila taasisi kuwasilisha kwenye ofisi yangu taarifa ya ushiriki wake katika maadhimisho ya wiki ya Utumishi wa Umma mara baada ya maadhimisho haya kumalizika. Taarifa hizo zitaisaidia Ofisi yangu kuona ninichakufanyai kuboresha zaidi maadhimisho haya,” alisema Waziri Simbachawene.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa taasisi zinazoshiriki maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2024 yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park ambayo yamebebwana kaulimbiu isemayo, “Kuwezesha kwa Utumishi wa Umma Uliojikita kwa Umma wa Afrika ya Karne ya 21 iliyojumuishi na inayostawi; Ni safari ya Mafunzo na mabadiliko ya Teknolojia.”

Katika maadhimisho hayo jumla ya Wizara 14 na Taasisi za Umma 60 zinashiriki.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. George Simbachawene (Mb) akitoa hotuba ya ufunguzi wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2024 katika viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma tarehe 19 Juni, 2024.



WAZIRI SIMBACHAWENE AFUNGUA MAONESHU YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhizani Jakaya Kikwete (Mb) (kushoto) akipata maelezo kuhusu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Ajira na Maendeleo ya Walimu, Mwl. Mectildis Kapinga tarehe 19 Juni 2024, wakati kiongozi huyo alipotembelea banda la TSC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dkt. Grace Magembe akisaini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma.



Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Utawala Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi Apsa Othman (kushoto) akisalimiana na mmoja wa Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Musa Magufuli aliyetembelea banda la TSC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma tarehe 19 Juni, 2024.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Dodoma, Bi Kepha Weston Motela (kushoto) akitoa maelezo kwa mmoja wa Wakurugenzi kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bw. Musa Magufuli aliyetembelea banda la TSC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma tarehe 19 Juni, 2024.

WAZIRI SIMBACHAWENE AFUNGUA MAONESHU YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA



Wateja waliofika katika banda la TSC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma akipatiwa huduma.



Mwalimu aliyetembelea banda la TSC kwenye kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma akitoa maelezo yake kwa ajili ya kupatiwa huduma.

Baadhi ya washiriki waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma tarehe 19 Juni, 2024.



Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Ajira na Maendeleo ya Walimu Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Mectildis Kapinga (kushoto) akimsikiliza mteja aliyetembelea banda la TSC kwenye maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yanayofanyika katika Viwanja vya Chinangali jijini Dodoma

MWL. PAULINA: RAIS SAMIA AMEAMUA KUINUA KIWANGO CHA ELIMU NCHINI

Na Mwandishi wetu TSC – Tanganyika.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt Samia Suluhu Hasan alipongezwa kwa usimamizi mzuri wa sekta ya elimu nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu mipya ya elimu.

Pongezi hizo zilitolewa tarehe 18 Juni, 2024 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati wa mkutano na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri za Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi.

Alisema kuwa uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umedhamiria kuinua kiwango cha elimu nchini baada ya kuanza kuondoa changamoto mbalimbali ambazo zilikuwa zikiwakabili walimu ikiwemo kutopandishwa madaraja, kutolipwa malimbikizo yao ya mishahara, malipo ya madeni ya uhamisho, nauli na kukemea lugha zinazowavunja moyo



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali kuimba wimbo wa Taifa tarehe 18 Juni, 2024 wilayani Tanganyika wakati wa mkutano wake na walimu wa shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya hiyo.

walimu.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa Rais Samia amekuwa msimamizi imara wa sekta ya elimu na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri kwa wanafunzi kujifunza na walimu kufundisha kupitia mradi wa SEQUIP, BOOST na UVIKO.

"Tunampongeza Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweka

utaratibu mzuri katika sekta ya elimu, miundombinu inajengwa lakini pia walimu na mazingira ya kujifunzia yameboreshwa... Rais anathamini sana michango ya walimu katika maendeleo ya elimu nchini," alisema.

Aliongeza kuwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeamua kuweka mazingira ambayo wanafunzi wote wanapata elimu katika mazingira mazuri.

Kufuatia jitihada kubwa zilizofanywa na Rais za kuinua kiwango cha elimu, Mwl. Paulina aliwataka walimu kuunga mkono juhudi hizo kwa kutokubali elimu iporomoke kwa kuhakikisha wanasimama katika nafasi zao kwa weledi na kuongeza ubunifu wanapofundisha.

"Hakuna mtoto mjinga wala asiye fundishika, ni jukumu letu la kuwasaidia kufikia malengo yao... Walimu wenzangu sisi ndio tuko katika usukani tusikubali elimu iporomoke mikononi mwetu... anguko lolote la elimu sisi ndio tutalaumiwa," aliwaasa.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akisisitiza jambo wakati akizungumza na Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Tanganyika tarehe 18 Juni, 2024.

MWL. PAULINA: RAIS SAMIA AMEAMUA KUINUA KIWANGO CHA ELIMU NCHINI



Watumishi wa TSC Wilaya ya Singida, Amos Kimu (kulia) na Mwalimu Flora Mushi (kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja katika ofisi za TSC Wilaya ya Singida hivi karibuni.



Watumishi wa TSC Wilaya ya Singida, Amos Kimu (kulia) na Mwalimu Flora Mushi (kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja katika ofisi za TSC Wilaya ya Singida hivi karibuni.

WALIMU MANYARA WAMPONGEZA RAIS SAMIA KWA KUSIKIA KILIO CHAO

**Na Mwandishi wetu -TSC
Manyara**

Walimu kutoka Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Manyara walingeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake za kutatua kero sita zilizokuwa zikiwakabili.

Walimu hao walitoa kauli hiyo katika nyakati tofauti walipokuwa kwenye Mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwana alipokuwa akieleza mikakati ya kuboresa ufundishaji kwenye Wilaya za Kiteto, Simanjiro, Mbulu, Babati na Hanang hivi karibuni.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Matui wilayani Kiteto, Dkt. Japhet Kivuyo alimshukuru Rais Samia kwa kuendelea kupandisha madaraja walimu, kulipa madai ya malimbikizo, nauli za likizo na ujenzi wa miundombinu ya madarasa ambayo imeweka mazingira mazuri ya kufundishia.

Alisema kuwa kiongozi huyo Mkuu wa Nchi alipokuwa akizungumza na Wakuu wa Shule za Tanzania Bara katika mkutano uliofanyika mkoani Mwanza aliahidi kushughulikia kero ya uhaba wa nyumba kwa walimu ili kuweka mazingira mazuri ya wao kutoa elimu kwa wanafunzi.

Akizungumza wakati wa mkutano huo, Mwalimu kutoka Shule ya Msingi Jitegemee Wilayani Simanjiro, Mwl. Abraham Kissimbi alisema kuwa Rais Samia alivyoanza kutatua kero zao amewaongezea nguvu katika kufundisha kwa kuwa amesikia kero ambazo zilikuwa zikiwasumbua.

Kwa upande wake, Mwl. Matheo

Bwaya alisema kuwa walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wanafarajika kwa uwepo wa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwani amekuwa akiwasemea walimu na kutatua changamoto zinazowabana katika maeneo yao ya kazi.

“Walimu wamefarajika kuwa mama anatupenda, anatuthamini na anatumia...Tunaoomba viongozi wa TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu kufikisha salamu kwa Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ...mwambieni nasi tunampenda,” alisema.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Tlawi katika Halmashauri ya Mbulu, Mwl. Faustini Suluo alisema kuwa wanapokea pongezi na salamu ya upendo alizozitoa mkoani Mwanza mwezi Desemba mwaka jana (2023) kwa moyo mkunjufu wakati wa kikao cha wakuu wa Shule nchini.

“Rais Samia tunampenda, tunatambua kazi yake nzuri ambayo wanaifanya walimu wa Nchi hii...sisi tunaendelea kumuunga mkono mama yetu na viongozi wengine wanaomsaidia,” alisisitiza.

Afisa Elimu wa Elimu ya Awali na Msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Mwl. Simon Mumbee alisema kuwa walimu wa Mbulu wanamshukuru sana Rais Mhe. Dkt. Samia kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha elimu nchini inakua na kuondoa changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu.

Alisema kuwa katika kipindi cha uongozi wake ameongeza nguvu katika kuimarisha kuwekeza

katika ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na Sekondari, jambo lililoongeza ari kwa walimu kufundisha na wanafunzi kujifunza.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwana alisema kuwa Rais Samia anawapenda, anawajali na kuwatathimini walimu na ndio maana aliagiza viongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhakikisha wanatatua changamoto zote zinazowakabili ili waweze kuwalea na kutoa ujuzi kwa wanafunzi wakiwa na amani moyoni.

Alisema kuwa kupitia agizo hilo Ofisi ya TAMISEMI kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi wa Walimu na Maafisa Utumishi katika Halmashauri zote Nchi walifanya uchambuzi na kubaini kuwa baadhi ya walimu wanakabiliwa na changamoto zikiwemo kuchelewa kupandishwa madaraja, wengine kuchelewa kulipwa malimbikizo ya mishahara (arrear) na kutolipwa kwa stahili za nauli za likizo kwa wakati.

Mwl. Paulina alisema kuwa changamoto nyingine zilizobainishwa na kikosi kazi kilichoundwa na Waziri wa TAMISEMI ni baadhi ya walimu kutolipwa fedha za uhamisho kwa wakati, kutobadilishiwa miundo ya kiutumishi mara baada ya kujiendeleza kimasomo na matumizi ya lugha mbaya kutoka kwa wasimamizi ambazo zinawakatisha tamaa walimu.

Alisema kuwa changamoto zote hizo, Serikali imeshazifanyia kazi na ndio maana baadhi yao wameshaanza kulipwa madai yao na kuongeza kuwa nia ya Serikali ni kufanya changamoto za walimu kuwa historia.

KATIBU TSC ASHIRIKI UFUNGUZI WA MASHINDANO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA MKOANI TABORA

Na Mwandishi wetu – Tabora.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama alishiriki Ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA uliofanyika tarehe 8 Juni, 2024 katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora.

Kabla ya ufunguzi huo uliofanywa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungani wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Katibu huyo wa Tume aliungana na wanafunzi katika maandamano ya kuingia uwanjani.

Ufunguzi wa mashindano hayo kwa mwaka huu yalikuwenda sambamba na maadhimisho ya Miaka 50 ya UMITASHUMTA ambapo kauli mbiu ya mashindano hayoni, "Miaka 50 ya UMITASHUMTA Tunajivunia Mafanikio katika Sekta ya Elimu, Michezo na Sanaa, Hima Mtanzania Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024."



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akibadilishana na Mawazo na Mbunge wa Urambo, Mhe. Magreth Sita wakati wa ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye miwani) akishiriki maandamano ya wanafunzi kuingia uwanjani katika ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.



KATIBU TSC ASHIRIKI UFUNGUZI WA MASHINDANO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA MKOANI TABORA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wanafunzi ambao pia ni wanamichezo ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (mwenye mizwani) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya viongozi walioshiriki ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.

Wanafunzi mbalimbali wakiwa kwenye ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.



Wanafunzi wakitoa burudani wakati wa ufunguzi wa mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA Kitaifa uliofanyika katika Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mkoani Tabora tarehe 8 Juni 2024.

Na Mwandishi Wetu – Mlele.

Walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlele mkoani Katavi waliazimia kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa juhudi kubwa kwa ajili ya kupandisha ufaulu baada ya kazi nzuri ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuonesha upendo kwao na kuanza kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili.

Afisa Taaluma Mkoa wa Katavi, Mwl. George Mtawa akisoma maazimo kwa niaba ya Walimu wa Wilaya ya Mlele kwenye mkutano baina yao na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama alisema kuwa Walimu hao wameazimia kufikia asilimia mia moja (100%) kwenye utoaji wa elimu katika ngazi zote za Elimumsingi na sekondari.

Alisema kuwa watahakikisha wanaongeza asilimia za watoto wa darasa la kwanza wanamudu kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) na kuongeza ufaulu kwa asilimia 100 kwa Upimaji wa Darasa la Nne, Mtihani wa Darasa la Saba, Upimaji wa Kidato cha Pili na Mtihani wa Kidato cha Nne na Sita.

Mwl. Mtawa aliongeza kuwa katika kufikia mafanikio hayo watajitahidi kubadili mtazamo kwenye mbinu za ufundishaji na kuwa wabunifu zaidi ili kuvuka lengo la kitaifa.

“Kwa kweli tunamshukuru Rais, mama yetu Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kusikia kilio chetu...sisi walimu wa Mlele tunaazimia kuchapakazi ambapo kwa upande wa Shule za Sekondari tunakusudia kuhakikisha kuwa ufaulu wa chini uwe ni daraja la III (Division III) na kuhakikisha hakuna mtoto wa darasa la kwanza asiyemudu KKK kwa kuweka msingi mzuri kwa darasa la kwanza na kwa upande wa Darasa la III wanafunzi waweze kumudu kusikiliza, kuongea, kusoma na kuandika lugha ya

KAZI NZURI YA RAIS SAMIA YAWAONGEZA NGUVU WALIMU MLELE



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani Mlele mkoani Katavi hivi karibuni.

kiingereza,” alisema.

Awali Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwana alisema kuwa kazi kubwa inaendelea kufanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha inatatua changamoto sita za walimu nchini.

Katibu huyo wa TSC alisema kuwa Serikali imedhamirisha kuhakikisha walimu wote wanaodai na wanaostahili wanalipwa madai yao yote.

Alizitaja changamoto za walimu kuwa ni ucheleweshwaji katika kupanda cheo/madaraja, kwalimu kutobadilishiwa cheo kwa wakati

baada ya kujiendeleza kielimu, madeni ya likizo, malimbikizo ya mshahara na fedha za uhamisho kutolipwa kwa wakati pamoja na baadhi ya vionozizi kuwa na lugha zisizoridhisha wakati wa kutoa kwa walimu.

Aidha, Mwl. Paulina aliwataka Walimu wilayani Mlele kuchapa kazi kwa bidii katika kuwalea watoto/wanafunzi ili kuwafanya kuwa na maadili mema, wazalendo, waadilifu na kuwa na utu mwema.

Alisema kuwa sanjari na hilo wanatakiwa kuchapakazi katika kuwapa ujuzi wanafunzi ili waweze kuwa wataalamu katika kada mbalimbali ambazo zitaendelea kuchochea maendeleo nchini.

KAZI NZURI YA RAIS SAMIA YAWAONGEZEA NGUVU WALIMU MLELE



Afisa Taaluma Mkoa wa Katavi, Mwl. George Mtawa akizungumza wakati wa mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu na walimu wa Wilaya ya Mlele hivi karibuni.



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani Mlele wakiimba wimbo wa Taifa wakati wa mkutano wao na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) (hayupo katika picha) uliofanyika hivi karibuni.



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wilayani Mlele wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) (hayupo katika picha) wakati wa mkutano wa Katibu wa Tume na walimu hao uliofanyika hivi karibuni.

WAJUMBE WA KAMATI YA TSC WILAYA YA ROMBO WAAPISHWA

Na Mwandishi wetu – Rombo.

Wajumbe wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo waliapishwa rasmi kutumikia Tume hiyo katika hafla iliyofanyika tarehe 19 Juni, 2024 kwenye Ofisi za Mkuu wa Wilaya ya

Rombo.

Uapisho huo ulifanywa na Hakimu Mwandamizi wa Mahakama ya Mwanzo Mashati, Mhe. Muhidini Rajab Daudi ambapo hafla ya uapisho huo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa elimu katika Wilaya hiyo akiwemo Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Maafisa wa Idara ya Elimu Msingi

na Sekondari pamoja na Ofisi ya Mthibiti Ubora.

Walioapishwa ni Mwenyekiti wa Kamati Mwl. Patricia Marandu, Bi Johari Athumani ambaye ni Katibu Tawala wa Wilaya ya Rombo, Mwl. Hussein Juma Hussein ambaye ni mwakilishi wa shule za Msingi na Mwl. Ally Babu Seif ambaye ni mwakilishi wa shule za Sekondari.



Menyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Mwl. Patricia Marandu akiapa kutumikia nafasi hiyo katika hafla ya uapisho wa Wajumbe wa TSC wa Wilaya hiyo, tarehe 19 Juni, 2024.



Mjumbe wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo ambaye pia ni Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Bi Johari Athumani (kushoto) akiapa kutumikia nafasi ya Mjumbe wa Kamati ya TSC katika Wilaya Rombo. Pembeni yake ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mashati, Mhe. Muhidini Rajab Daudi ambaye ndiye aliyewaapisha Wajumbe wa Kamati hiyo.



Mjumbe wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Mwl. Hussein Juma Hussein (mwakilishi wa shule za Msingi) akiapa kutumikia nafasi hiyo katika hafla ya uapisho wa Wajumbe wa TSC wa Wilaya Rombo iliyofanyika tarehe 19 Juni, 2024.



Mjumbe wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Mwl. Ally Babu Seif (mwakilishi wa shule za Sekondari) akiapa kutumikia nafasi hiyo katika hafla ya uapisho wa Wajumbe wa TSC wa Wilaya Rombo iliyofanyika tarehe 19 Juni, 2024.

WAJUMBE WA KAMATI YA TSC WILAYA YA ROMBO WAAPISHWA



Baadhi ya washiriki waliohudhuria hafla ya uapisho wa Wajumbe wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo iliyofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Rombo tarehe 19 Juni, 2024.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Bi. Zema Jamal akifanya utambulisho wakati wa hafla ya uapisho wa Wajumbe wa Kamati ya TSC Wilaya ya Rombo iliyofanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Rombo tarehe 19 Juni, 2024. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Mwenyekiti wa Kamati ya TSC Wilaya ya Rombo, Mwl. Patricia Marandu na kulia ni Hakimku Mwanzizi wa Mahakama ya Mwanzo Mashati, Mhe. Muhidin Rajab Daudi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Mwl. Patricia Marandu (wa tatu kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Kamati ya TSC Wilaya ya Rombo mara baada ya kuapishwa. Pichani, wa tatu kutoka kulia ni Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Rombo, Bi. Zema Jamal.



MWL. PAULINA: MAAFISA ELIMU WILAYA SHIRIKIANENI NA MAAFISA UTUMISHI KUTATUA KERO ZA WALIMU

Na Mwandishi wetu TSC – Mpanda.

Maafisa Elimu Wilaya ya Nsimbo na Mpanda walitakiwa kushirikiana na Maafisa Utumishi katika maeneo yao kwa ajili ya kujiridhisha kama taarifa za madai yanayohusu malimbikizo ya mishahara ya walimu hayana kasoro na hoja ili stahili zao ziweze kulipwa.

Kauli hiyo ilitolewa tarehe 18 Juni, 2024 na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama wakati wa mkutano na walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri za Wilaya ya Nsimbo na Mpanda mkoani Katavi uliolenga kuweka mikakati na mbinu za kuongeza ubora katika kutoa elimu kwa wanafunzi.

Alisema kuwa endapo wataona kuwa katika ujazaji wa taarifa

za madai ya walimu zina hoja ni vema wakashirikiana na Maafisa Utumishi kurekebisha kasoro hizo ili walimu waweze kulipwa madai yao kwa wakati.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umedhamiria kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma wakiwemo walimu na hivyo ni jukumu la wasimamizi wao kuweka mazingira ambayo yatakuwa hayawafanyi kusubiri kwa muda mrefu.

Alisema kuwa katika ufuatiliaji Walimu wanatakiwa kupata majibu kutoka kwa Maafisa Elimu kwa kuwa ndio wasimamizi wao juu ya hatua ambayo imefikiwa katika kushughulikia madai yao badala ya kuwasukuma kufuatilia wenyewe kwa Maafisa Utumishi ambao wakati mwingine wanakutana na majibu yanayowavunja moyo.

“Ninyi Maafisa Elimu ni Wakuu wa Idara kama walivyo Maafisa Utumishi wa Wilaya, nendeni mkae nao na kuhakikisha jina moja baada ya jingine na ikibainika wapo wenye changamoto saidieni kutatua badala ya kuwafanya walimu kusubiri arrears mwaka wa kwanza unakwisha, bila mafanikio, mwaka wa pili na mwaka wa tatu unakwisha bila kulipwa kwa sababu ya uzembe unaotokana na kutojibu hoja za kiutumishi ikiwemo kukosekana kwa baadhi ya nyaraka,” alisema.

Alisema kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipanga kuhakikisha inalipa arrears zote za walimu na ndio maana kwa upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imelipa walimu 211 na wanaodai ni 25 ambao nao baada ya kukamilika kwa taarifa zao watalipwa.

HABARI KATIKA PICHA



Washiriki mbalimbali waliotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vua Chinangali Park jijini Dodoma.



Washiriki mbalimbali waliotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja vua Chinangali Park jijini Dodoma.

MWL. PAULINA: TUMIENI LUGHA NZURI MNAPOTOA HUDUMA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu –
Mpimbwe.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama aliwataka viongozi kuacha kutoa lugha zinazowakwaza walimu wanapokuwa wamekwenda kwenye Ofisi za Halmashauri kufuatilia masuala yao ya kiutumishi.

Alitoa kauli hiyo hivi karibuni wakati wa mkutano wake na Walimu kutoka Halmashauri ya Mpimbwe kwa lengo la kufanya ufuatiliaji hali ya utoaji elimu kwa wanafunzi, kujadiliana na walimu mbinu bora za ufundishaji pamoja na kuwapongeza walimu wa Halmashauri hiyo kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya katika kutoa huduma kwa wanafunzi.

Mwl. Paulina alisema kuwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unawapenda na kuwathamini sana walimu na hivyo walimu



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akiwaongoza viongozi mbalimbali wa Halmashauri ya Mpimbwe kuimba wimbo wa Taifa tarehe 19 Juni, 2024 wakati wa mkutano na walimu wa shule za Msingi na Sekondari.

hawapaswi kufanyiwa vitendo vinavyowakatisha tamaa ikiwepo kuwajibu kwa lugha inayowakwaza.

Alisema kuwa walimu wanapokwenda kwenye Ofisi za Halmashauri kufuatilia masuala yao ni vyema wakakaribishwa kwa upendo na kupewa huduma stahiki kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu na sio kwa matakwa ya

kiongozi.

Mwl. Paulina aliongeza kuwa ni muhimu viongozi wanaowahudumia walimu wakiwemo Maafisa Elimu na Maafisa Utumishi kuelewa kuwa nafasi walizonazo ni dhamana ambayo wamekasimiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo wanapaswa kuitumia kwa kutoa huduma nzuri kwa wananchi na walimu.

“Hizi nafasi tulizo nazo ni sawa na makoti tuliyoazimwa siku mwenyewe akilichukua tutarudi katika nafasi zetu za awali... Maafisa Elimu tunapotoa huduma kwa walimu ni vema tukatambua kuwa nasi ni walimu na hivyo nafasi tulizonazo tumepewa kuhakikisha tunamsaidia Rais kutoa huduma nzuri kwa wale tunaowatumikia,” alisema.

Alisema kuwa walimu ndio chimbuko la kada zote nchini na duniani kote ni vema wakathaminiwa kama vile ambavyo viongozi wakuu hapa nchini wanavyowapenda, kuwathamini, kuwajali na kutatua changamoto zao.



Baadhi ya walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wa Halmashauri ya Mpimbwe wakiimba wimbo wa Taifa wakati wa mkutano wa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (hayupo katika picha) tarehe 19 Juni, 2024.

TSC YASHIRIKI KLINIKI YA KUTOA MSAADA NA USHAURI WA KISHERIA

Na Mwandishi Wetu – Dodoma.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inashiriki Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria inayoratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Mawakili wa Serikali inayofanyika tarehe 26 Juni – 03 Julai, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Kliniki hiyo ilifunguliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi tarehe 26 Juni, 2024 ambapo alisema kuwepo kwa Kliniki hiyo ni sehemu ya kutekeleza maagizo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosisitiza kuwatumikia wananchi.

Aliongeza kuwa utoaji wa Msaada na Ushauri wa kisheria kwa wananchi yanaunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameelekeza viongozi mbalimbali wa Serikali kushughulikia kero na changamoto za wananchi.

“Pamoja na maelekezo ya kiongozi wetu, Mkuu wa Nchi tukio hili pia linalenga



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi akitoa hotuba ya ufunguzi wa Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 26 Juni, 2024.

kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya kutoa elimu na ushauri juu ya masuala ya kisheria kwa wananchi katika nyanja zote,” alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Aliongeza kuwa Kliniki hiyo inalenga kupunguza na kuepusha migogoro miongoni mwa wananchi na isiposhughulikiwa kwa wakati inaweza kuleta

migogoro, kukosekana kwa haki na kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi.

“Mtu anapokuja na kusemezana na maafisa wetu, sisi tunaongeza thamani ya kuhakikisha tunaepusha na kupunguza migogoro ambayo isiposhughulikiwa kwa wakati itaishia kwenda mahakamani ambapo kuna gharama ya muda na ushindani wa haki, maana mahakamani ni pande mbili zinashindania haki” alisema Dkt. Feleshi.

Aliongeza kuwa, “tuna wajibu wa kudumisha utawala bora na misingi yake kwa sababu lengo la Serikali ni kuona kuna ustawi wa jamii, yaani watu wanafurahia kupata huduma iliyo bora na inayotolewa kwa wakati.”

Alisema Kliniki hiyo inakusudia kuingeza mtengamano, utulivu na kuchochea maendeleo ya jamii ili kufanya wananchi wafanye shughuli zao za kujiletea maendeleo kwa amani.

“Mahali pasipokuwa na usikilizano, yaani kuwepo namna ya kujadili changamoto au kero kunakuwa na fukuto na madhara yake ni kufanya maendeleo yasifikwiwe kwa wakati uliokusudiwa. Kukiwa na uadui watu hawawezi kupata haki zao, hivyo tunaamini kuwa wananchi watakaokuja kupata huduma hapa itawasaidia kuepusha gharama nyingi,” alisema kiongozi huyo.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) nayo imeweka banda katika Kliniki hiyo ili kuhakikisha inatoa huduma za kisheria zinazohusu masuala ya Utumishi wa Walimu kwa walimu na wadau wengine ikiwa ni sehemu ya kutekeleza agizo la viongozi mbalimbali la kuhakikisha kero na changamoto za walimu zinatatuliwa ili walimu waendeleo kufundisha shuleni wakiwa na utulivu.

Watoa huduma katika banda la TSC ni pamoja na Maafisa Sheria kutoa Kitengo cha Huduma za Kisheria, Wakili Josephine Chilongozi na Wakili Selina Magoiga.



Viongozi mbalimbali (meza kuu) waliohudhuria hafla ya ufunguzi wa Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 26 Juni, 2024 wakiwa katika hali ya utulivu.

TSC YASHIRIKI KLINIKI YA KUTOA MSAADA NA USHAURI WA KISHERIA



Maafisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Josephine Chilongozi (kulia) na Wakili Selina Magoiga (kushoto) wakimsikiliza mteja aliyetembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria tarehe 26 Juni, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (wa pili kutoka kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na wanasheria mbalimbali wanaotoa huduma katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria inayofanyika tarehe 26 Juni – 03 Julai, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.



Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa TSC (waliosimama) wanatoa huduma katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria inayofanyika tarehe 26 Juni – 03 Julai, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Wateja waliotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria tarehe 26 Juni, 2024 katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma wakipatiwa huduma.

MWL. PAULINA: WASAIDIENI WALIMU WAPATE MIKOPO KATIKA TAASISI HALALI

Na Mwandishi Wetu – MPANDA.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Mwl. Paulina Nkwama aliwataka viongozi wa Halmashauri za Mkoa wa Katavi kutoa taarifa kwa walimu juu ya fursa ya kupata mikopo kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi wa Watumishi wa Umma (ESS) ulioanzishwa na Serikali kupitia dirisha la mikopo.

Alitoa kauli hiyo tarehe 20 Juni, 2024 kwenye mkutano wa majumuisho na viongozi kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Katavi mara baada ya kumaliza ziara ya kikazi ya kukutana na walimu kwa ajili ya kukumbushana mbinu za kuboresha ufundishaji ili kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari.

Mwl. Paulina alisema kuwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akizungumza na viongozi wa Elimu kutoka Halmashauri mbalimbali za Wilaya za Mkoa wa Katavi jana wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara yake ya kikazi.

ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan imeingia mkataba na baadhi ya Benki za hapa nchini kwa ajili ya kuwawezesha kupata mikopo kwa riba nafuu.

Aliongeza kuwa walimu

wamekuwa wakidhalilishwa na baadhi ya watu ambao wamekuwa wakiwakopesha kupitia mikopo umiza ambayo inawafanya wakabidhi kadi zao za kibenki na kupangia matumizi ya fedha na wakopeshaji ambao hawakuruhusiwa na hawana vibali vya Benki Kuu ya Tanzania.

“Serikali ya Awamu ya Sita imeweka wazi fursa kwa watumishi kupata mikopo ya Benki na ile ya Hazina wasaidieni walimu kukopa katika Benki ambazo zimeingia mkataba na waajiri... mikopo ya Hazina iwafikie walimu, viongozi wa Halmashauri, wasaidieni walimu jinsi ya kujaza fomu na hatimaye nao waweze kupata,” alisema.

Mwl. Paulina alisema Serikali imeanzisha dirisha hilo ili kuwafikia watumishi wengi wenye uhitaji wapate mikopo.

Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Utawala na Utumishi, Bi. Cresencia Joseph alisema kuwa watumishi wanaohitaji mikopo ya Hazina wanatakiwa kuingia dirisha Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi kwa Watumishi wa Umma na kujaza fomu kwa ajili ya kuomba mikopo.



Baadhi ya Viongozi wa Elimu kutoka Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Katavi wakimsikiliza Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama.

MWL. PAULINA: WASAIDIENI WALIMU WAPATE MIKOPO KATIKA TAASISI HALALI



Katibu Tawala Msaidizi anayeshughulikia Utawala na Utumishi, Bi. Cresencia Joseph akitoa ufafanuzi kwa Viongozi wanaosimamia sekta ya elimu kutoka Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Katavi wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara ya kikazi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika tarehe 20 Juni, 2024.



Kaimu Afisa Elimu Mkoa wa Katavi, George Mtarwa akitoa ufafanuzi kwa viongozi wanaosimamia sekta ya elimu kutoka Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Katavi wakati wa kikao cha majumuisho ya ziara ya kikazi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kilichofanyika tarehe 20 Juni, 2024.

MWL. PAULINA AUNGANA NA VIONGOZI MBALIMBALI KUSHIRIKI MAZISHI YA TIXON NZUNDA

Na Mwandishi wetu TSC – Songwe.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama aliungana na Viongozi kutoka maeneo mbalimbali nchini kushiriki mazishi ya aliyekuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro marehemu Tixon Nzunda.

Mazishi yalifanyika katika Kijiji cha Msinda, Kata ya Mpemba mkoani Songwe na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Naibu Waziri wa Ujenzi Injinia, Mhe. Godfrey Kasekenya, Naibu Waziri wa Kilimo, Mhe. David Silinde, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Daniel Chongolo, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Peter Serukamba, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhe. Antony Mtaka na aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Mhe. Godfrey Zambi.

Viongozi wengine ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Bw. Adolf Ndunguru, Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu Mstaafu wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Tawala Mstaafu wa Mkoa wa Singida, Mwl. Doroth Mwaluko, Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Rehema Madenge na Katibu Tawala Mkoa wa Mara, Bw. Msalika Makungu.

Akitoa salamu za Chama, Dkt. Nchimbi alisema kuwa marehemu alikuwa muadilifu, mkweli, mwenye msimamo asiyependa kuyumbushwa na mchapakazi aliyeipenda Nchi yake.

Aliwatakawatendajikuhakikisha



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akisaini kitabu cha maombolezo cha msiba wa aliyekuwa Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro marehemu Tixon Nzunda alipoungana na viongozi katika mazishi ya kiongozi huyo.

wanaiga mfano wa marehemu Nzunda katika kuwatumikia wananchi kwa kutoa huduma kwa uadilifu na kuchapa kazi kwa bidii ili kuwaletea maendeleo wananchi.

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu alisema kuwa msiba huo umewaumiza wakazi wa Kilimanjaro na watumishi kutokana na jinsi alivyojenga daraja na ushirikiano mzuri na wananchi.

Alisema kuwa kwa wakazi na watumishi wa Mkoa wa Kilimanjaro itachukua muda mrefu kumsahau marehemu Tixon kutokana na utumishi wake uliotukuka.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Daniel Chongolo alisema

kuwa marehemu Nzunda alikuwa Mwalimu wa uadilifu, ukweli, uchapa kazi, uzalendo na mwenye msimamo usioyumbushwa ili mradi atambue kuwa yuko sahihi.

Aliwataka viongozi na watumishi kuchukua somo ambalo wanapaswa kuchukua wakati wanapotoa huduma kwa wananchi wanaowatumikia.

Mtoto wa marehemu, Victor Tixon Nzunda alisema kuwa baba yao amewaachi mafundisho mengi ikiwemo kumcha Mungu kwa bidii, kuchapa kazi kwa bidii na kuwaheshimu watu wote bila kujali umri, dini au hali yake ya kipato.

MWL. PAULINA AUNGANA NA VIONGOZI MBALIMBALI KUSHIRIKI MAZISHI YA TIXON NZUNDA



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kushoto) akibadilishana marwazo na Katibu Tawala Mstaafu wa Mkoa wa Singida Mwl. Doroth Mwaluko (katikati), Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mhe. Daniel Chongolo (kulia) waliposhiriki mazishi ya aliyekuzwa Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro Tixon Nzunda.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akibadilishana marwazo na Katibu Tawala Mstaafu wa Mkoa wa Singida Mwl. Doroth Mwaluko (kulia), Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Rehema Madenge (kushoto) waliposhiriki mazishi ya aliyekuzwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro, Tixon Nzunda.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akibadilishana marwazo na Katibu Tawala Mstaafu wa Mkoa wa Singida Mwl. Doroth Mwaluko (katikati), Katibu Mstaafu wa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora Dkt. Laurean Ndumbaro (kushoto) waliposhiriki mazishi ya aliyekuzwa Katibu Tawala Mkoa wa Kilimanjaro Tixon Nzunda.

MWL. NKWAMA ATEMBELEA KLINIKI YA HUDUMA NA USHAURI WA KISHERIA, AHUDUMIA MTEJA KWA NJIA YA SIMU

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama tarehe 27 Juni, 2024 alitembelea Kliniki ya Kutoa Msaada na Ushauri wa Kisheria inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma.

Mwl. Nkwama alitembelea mabanda ya ofisi mbalimbali zinazotoa huduma katika kliniki hiyo ikiwemo banda la TSC ambapo alipitia daftari lililoorodhesha hoja za wateja wanaokuja kuhudumiwa na TSC ambapo aliekeza maafisa wanaotoa huduma katika banda hilo kuhakikisha hoja zote zinashughulikiwa na wateja hao wanapatiwa mrejesho.

“Ninawapongeza kwa namna mnavyoendelea kupokea wateja na kuwahudumia. Nimepitia hoja zote nimeona wapo walimu kutoka nje ya Mkoa wa Dodoma wamekuja hapa na kuandika changamoto zao, ninajua mmewapatia majibu lakini zipo hoja zinazohitaji uchambuzi wa kina ili kuhakikisha mwalimu



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akipitia hoja za wateja waliotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Huduma na Ushauri wa Kisheria katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 27 Juni, 2024.

anapata kile anachostahili. Ninataka hoja hizi ziwasilishwe Ofisi za TSC katika Wilaya walimu hao wanapotoka ili kila Katibu Msaidizi atoe majawabu na walimu wapate majibu ya hoja zao,” alisema Mwl. Nkwama.

Aliongeza kuwa TSC imeshiriki kliniki hiyo ikiwa ni mwendelezo wa azma yake ya kuhakikisha

inatumia kila fursa inayopatikana ya kukutana na walimu ili kusikiliza na kutatua changamoto zao kama Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan inavyoelekeza.

“Kama mnavyofahamau Serikali yetu imejikita kuhakikisha kuwa changamoto za walimu zinatatuliwa ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa utulivu. Tumepanga kila fursa inayopatikana ya kukutana na walimu ni lazima tushiriki ili tuendeleo kutatua changamoto zao. Kila mwalimu anayekuwa hapa kuwasilisha changamoto yake ni lazima tuifanyie kazi ili iishe sio kumpatia majibu ya juu juu tu,” alisisitiza Mwl. Nkwama.

Akiwa katika banda hilo la TSC, Mwl. Nkwama alipata fursa ya kumhudumia mteja kwa njia ya simu na kumpatia ufumbuzi wa changamoto aliyoivasilisha.

Kliniki hiyo inayoratibiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Chama cha Mawakili wa Serikali ilianza tarehe 26 Juni, 2024 hadi tarehe 03 Julai, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akimsikiliza mteja kwa njia ya simu wakati alipotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Huduma na Ushauri wa Kisheria inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 27 Juni, 2024. Pembuni yake ni Afisa Sheria wa TSC, Wakili Josephine Chilongozi.

**MWL. NKWAMA ATEMBELEA KLINIKI YA HUDUMA NA USHAURI
WA KISHERIA, AHUDUMIA MTEJA KWA NJIA YA SIMU**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akitoa maelezo kwa mteja kwa njia ya simu wakati alipotembelea banda la TSC katika Kliniki ya kutoa Huduma na Ushauri wa Kisheria inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 27 Juni, 2024. Pembeni yake ni Afisa Sheria wa TSC, Wakili Josephine Chilongozi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati) akizungumza na Afisa kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili Silinde Gumada wakati alipotembelea Kliniki ya kutoa Huduma na Ushauri wa Kisheria inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 27 Juni, 2024. Pembeni yake ni Afisa Sheria wa TSC, Wakili Josephine Chilongozi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (wa pili kutoka kushoto) akizungumza na baadhi ya washiriki wa Kliniki ya kutoa Huduma na Ushauri wa Kisheria inayofanyika katika Viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma tarehe 27 Juni, 2024.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz